

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Ref.No.JA.9/259/01/A/49

15 Machi, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya Wizara ya Kilimo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi **tatu(03)** kama zilizyoainishwa katika tangazo hili.

1.0 MWAJIRI:WIZARA YA KILIMO

1.0.1 AFISA KILIMO DARAJA LA II- (NAFASI 3)

1.0.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kudhibiti visumbufu vya mazao na mimea;
- ii. Kukusanya takwimu za bei na mazao kila wiki na kila mwezi;
- iii. Kukusanya takwimu za upatikanaji mazao katika masoko kila wiki/kila mwezi;
- iv. Kuendesha mafunzo ya wataalam wa kilimo;
- v. Kufanya ukaguzi wa ubora na matumizi ya pembejeo na zana;
- vi. Ufuatiliaji wa mwenendo wa soko la mazao ya biashara;
- vii. Kuendesha mafunzo juu ya hifadhi bora ya udongo na maji;
- viii. Kutoa habari juu ya teknolojia mpya kwa wadau;
- ix. Kuandaa/kuandika taarifa za utekelezaji kwa sekta ndogo ya mazao;
- x. Kusimamia/kuendeleza taaluma ya uzalishaji mboga, matunda, maua na mazao mengine;
- xi. Kusimamia/kuendeleza uzalishaji wa mbegu bora;

- xii. Kuandaa, kutayarisha, kufunga na kusambazambegu bora;
- xiii. Kufanya majaribio ya magonjwa kwenye mbegu;
- xiv. Kufanya ukaguzi wa mbegu mpya kwa kushirikiana na watafiti wa mbegu kabla ya kupitishwa;
- xv. Kuendesha mafunzo ya kuzalisha mboga, mauwa na viungo;
- xvi. Kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya bustani;
- xvii. Kufanya utafiti mdogo mdogo wa mazao yanayofaa kulimwa katika sehemu ya kilimo cha umwagiliaji;
- xviii. Kufanya utafiti wa udongo;
- xix. Kuhamasisha uanzishaji wa vikundi vya wakulima/wamwagiliaji;
- xx. Kuzalisha mbegu za msingi baada ya kuzalishwa na watafiti;
- xxi. Kuendesha/kusimamia vishamba vya majaribio vya mbegu na uchunguzi maabara ili kuondoa utata juu ya mbegu;
- xxii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

1.0.3 SIFA ZA MWOMBAJI

Wahitimu wenye Shahada ya Kilimo au Shahada ya Sayansi waliojiimarisha katika mchepuo wa Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine au Vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali.

1.0.4 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani **TGSD**.

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizo nazo, wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitoshela (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini(**referees**) watatu wakuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo

- mbalimbali kwakuzingatia sifa za kazi husika.
- Postgraduate/Degree/AdvancedDiploma/Diploma/Certificates.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IVna VI
 - Computer Certificate
 - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards).
- vi. **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita(FORM IVAND FORM VIRESULTS SLIPS)HAVITAKUBALIWA.**
- vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika(TCU,NECTA na NACTE).**
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka NaCAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- x. Uwasilishaj iwa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xi. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 28 Machi,2022.**

Muhimu:Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

KATIBU OFISI YA RAIS
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA
S.L.P 2320
DODOMA

xii. *Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira(Recruitment*

Portal) kupitia anuani ifuatayo;

<http://portal.ajira.go.tz/>

(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘Recruitment Portal’)

xiii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili
HAYATAFIKIRIWA**

Limetolewa na;

**NAIBU KATIBU
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**